# TAARIFA YA ASASI ZA KIRAIA(AZAKI) KWA VYOMBO VYA HABARI

# UCHAMBUZI WA RIPOTI YA TUME YA JAJI CHANDE KUHUSU MATUKIO YA OKTOBA 2025

27 Aprili 2026, Dar es Salaam

## 1.0 Utangulizi

**Ndugu waandishi wa habari**

Asasi za Kiraia na Watetezi wa Haki za Binadamu tunajukumu kubwa katika jamii la kulinda na kuteta haki za binadamu pamoja na kufuatilia maswala ya uwajibikaji na utawala bora. Baada ya Tume iliyoundwa na Rais Samia Suluhu ya kuchunguza matukio yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2025 kutoa taarifa yake hadharani tarehe 23/4/2026, tumeona tunawajibu wa kuichambua na kutoa taarifa fupi kwa umma juu ya uchambuzi wa awali wa taarifa hii. Taarifa hii inalenga zaidi kuonesha mapungufu yaliyojitokeza katika taarifa hii na pia kutoa mapendekezo nini kifanyike.

Pamoja na kwamba toka awali hatukukubaliana na muundo wa tume hii ambao haukuzingatia ushirikishwaji wa makundi yote ya kijamii na wataalamu wa kimataifa wa uchunguzi wa matukio ya namna hii, bado tunawajibu pia wa kuchambua taarifa hii na kutoa mapungufu yake na kutoa mapendekezo yetu.

**Ndugu Wana Habari**

Kwa mujibu wa taarifa ya Tume, zifuatazo zilikuwa hadidu za rejea na mawanda ya Tume:

- **i.** Kuchunguza na kubaini chanzo halisi cha ghasia zilizotokea wakati wa uchaguzi mkuu wa Oktoba 2025 na siku chache zilizofuata,
- **ii.** Kuchunguza lengo kuu lililokusudiwa na wahusika katika kupanga na kutekeleza vitendo hivyo vya ghasia na uvunjifu wa amani.
- **iii.** Kuchunguza na kubaini madhara yaliyotokea kutokana na ghasia hizo, ikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu pamoja na madhara ya kiuchumi na kijamii,
- **iv.** Kuchunguza mazingira na hatua zilizochukuliwa katika kubaini na kukabiliana na ghasia zilizojitokeza,

**v.** Kupendekeza maeneo yanayohitaji kuimarishwa zaidi ili kuongeza uwajibikaji wa viongozi na raia kwenye kulinda amani, utawala wa sheria, haki za binadamu, utawala bora na mfumo madhubuti wa majadiliano ya kisiasa, kijamii, kiuchumi hadi kufikia maridhiano ya kitaifa na kuhakikisha matukio kama hayo hayatokei tena,

**vi.** Kuchunguza jambo lolote ambalo Tume itaona kuwa ni muhimu na linaendana na majukumu yake.

## 2.0 Mambo ya Msingi na Kasoro na Tulizobaini katika Taarifa hii

Uchambuzi wetu umebaini kuwa yapo baadhi ya mambo ya msingi ambayo sio mageni kwa umma ambayo Tume imeyaeleza lakini pia zipo kasoro nyingi katika taarifa hii ambayo tunatumia nafasi hii kuzichambua na kutoa mapendekezo.

Kwa mujibu wa hotuba ya Mwenyekiti wake, Tume imeainisha vyanzo vikuu vitano (5) kama vyanzo vikuu vya maandamano ya Oktoba 29, 2025. Mambo yote haya yameshawaelezwa katika taarifa nyingi za awali na pia asasi za kiraia mara zote tumekuwa tukisisitiza na kushauri kuwa madai haya yafanyiwe kazi. Hivyo, kwa Tume hii kutambua mambo haya kama ni vyanzo vya wananchi kuandamana na kudai yafanyiwe kazi ni kati ya mambo ambayo Tume imedhihirisha masuala muhimu ya muda mrefu ambayo yamekuwa ni madai ya wananchi.
Vyanzo hivyo vilivyotajwa ni kama ifuatavyo;

a) Masuala ya Kisiasa yanayojumuisha madai ya Katiba mpya, demokrasia katika mfumo wa vyama vingi, malalamiko ndani ya vyama vya siasa, madai ya maboresho ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na mfumo mzima wa uchaguzi,
b) Masuala ya kiuchumi yanayojumisha ugumu wa maisha, ukosefu wa ajira na kukosekana kwa usawa katika fursa za ajira na za kiuchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji yasiyo rafiki, utitiri wa kodi na tozo na mfumo usio rafiki wa utozaji na ukusanyaji,
c) Masuala ya kijamii yanayojumuisha mmomonyoko wa maadili na kushuka kwa uzalendo, kutopatiwa ufumbuzi na majibu stahiki kwa kero katika jamii kama vile rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na madai ya utekaji na kupotea kwa watu,
d) Utendaji usioridhisha wa baadhi ya watendaji na watumishi wa umma hususan ngazi za chini (Mamlaka za Serikali za Mitaa) ikiwa ni pamoja na kutosikilizwa au kutatua kero za wananchi kwa wakati na utekelezaji hafifu wa mapendekezo wa Tume zilizoundwa,
e) Masuala yanayohusu uhusiano wa kimataifa katika dunia ya leo na ijayo ambapo mataifa mengi yanatanguliza mbele maslahi yao kama

msingi wa mahusiano na kujaribu mbinu na mikakati mbalimbali ya kujiweka katika nafasi nzuri kuendeleza maslahi yao katika nchi nyingine hasa zinazoendelea na zenye rasilimali nyingi

### 2.1 Kasoro Tulizobaini

#### i. Kasoro kwenye mbinu za kukusanya taarifa za uchunguzi

Mwenyekiti anaeleza kuwa Tume ilitumia mbinu/methodolojia ya kukusanya taarifa kutoka kwenye vyanzo rasmi (official sources) yaani polisi, vituo vya afya au mahospitali. Lakini katika mgogoro wote, kwa vitendo vyake, polisi wanatambuliwa kama wahusika wakuu na wanatuhumiwa kwa kuua raia. Aidha, katika hatua ya awali kabla Tume haijaanza kuzuia vyambo vya habari kuripoti taarifa za wahanga, umma uliona jinsi polisi walivyokuwa wanaingilia na kushurutisha utendaji kinyume na weledi unaotakiwa kwenye mahospitali/vituo vya afya. Katika mazingira hayo, Tume kutumia taarifa za Polisi au wadau wake kupata taarifa badala ya kufanya uchunguzi wa kujitegemea haikuwa mbinu/methodolojia sahihi, yenye kuasili taarifa zinazoaminika.

Polisi na vyombo vya usalama vingine vinalamikiwa kuua, kuteka, kuondoa miili ya watu au majeruhi kwenye vituo vya afya na mahospitali na kuipeleka kusikojulikana, hivyo haiwezi kuwa chanzo cha kuaminika katika uchunguzi unaohusu masuala nyeti yanayohusu kukiukwa kwa haki za binadamu, hususani kuteka, kuua na kutesa raia.

Aidha, uchunguzi ni sayansi, hivyo Tume ilipaswa kufanya uchunguzi kisayansi. Kwa hiyo, kwa uchambuzi wetu, tunasema kwa ujasiri kuwa mbinu ya uchunguzi iliyotumiwa na Tume kukusanya taarifa za awali (primary & secondary data) haikidhi haja ya sifa za kisayansi za kuchunguza matukio ya Octoba 29, 2025.

#### ii. Tume kushindwa kubainisha waliozembea kupelekea yaliyotokea

Kwa muda mrefu watetezi wa haki za binadamu na masuala ya demokrasia, uchaguzi, utawala wa sheria na utawala bora tumeshauri ama kupitia maandiko ya kisomi, makongamano au mikutano na watendaji mbalimbali wa Serikali juu ya umuhimu na ulazima wa Serikali kutekeleza masuala ambayo Tume imeyaita kama vyanzo vya ghasia lakini isivyo bahati Serikali imekuwa ikipuuza maoni ya wadau.

Mtakumbuka hata kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika tulishauri ulazima wa kuifumua mifumo yetu ya uchaguzi ikiwemo uwezekano wa kupata Katiba mpya ili kuliokoa Taifa na machafuko lakini Serikali haikuwa tayari ama

kusikiliza, au kutekeleza maoni yetu, hata hivyo hatukukata tamaa tuliendelea kuishauri Serikali bila mafanikio. Hata hivyo, kwa uchambuzi wetu, yote yaliyotokea, kwa sehemu kubwa yamechangiwa na serikali kutokuchukua au kutokutekeleza maoni ya wadau kwani kama Tume ilivyotaarifu, madai hayo yamekuwepo kwa muda mrefu katika jamii yetu lakini yamekuwa yakipuuzwa. Taarifa ya Tume haijaelezea tatizo hili na tasisi pamoja na viongozi walishindwa kufanyia kazi hoja hazi hadi kupelekea yaliyotokea.

### iii. Tume imeshindwa Kuwataja Watanzania waliohusika

Pamoja na Tume kubainisha baadhi ya vichocheo vya matukio hayo; hata hivyo, katika taarifa yake, Tume imeonekana kuwa na kigugumizi katika kuwataja waliohusika na kupendekeza hatua za kuchukuliwa dhidi yao. Kwa mfano, Tume imekiri kuwepo kwa vitendo vya utekaji na kupotea kwa watu, na hata kutoa takwimu kuwa takribani watu 700 hawajulikani walipo hadi sasa. Pamoja na uzito wa suala hili, Tume haijaweza kueleza kwa kina nani wanaohusika na vitendo hivyo, wala nani anayetoa amri ya utekelezaji wake.

Kwa uchambuzi wetu, taarifa hii haiwezi kuonekana kuwa kamili kwa mujibu wa hadidu za rejea zilizoiunda Tume, ambazo zilielekeza kuchunguza lengo kuu lililokusudiwa na wahusika katika kupanga na kutekeleza vitendo hivyo vya ghasia, pamoja na kubaini chanzo halisi cha ghasia hizo. Ni vigumu kufikia malengo haya bila kuwataja waliohusika na bila kupendekeza hatua mahsusi za kuchukuliwa dhidi yao.

### iv. Uwepo wa Makambi na Mafunzo

Taarifa ya Tume imeeleza kuwa takribani watu 500 ya waliohusika na vitendo vya ghasia walipata mafunzo maalum kwa muda wa takribani wiki mbili. Hata hivyo, pamoja na madai haya mazito, uchunguzi wa Tume umeshindwa kubainisha kwa kina mafunzo hayo yalitolewa na nani na yalifanyika katika eneo gani mahsusi, licha ya kutaja kuwepo kwa kituo cha mafunzo jijini Dar es Salaam ambacho kipo umbali mfupi kutoka kituo kimoja cha polisi. Hali hii inaacha maswali mengi bila majibu kuhusu uhalisia na uthibitisho wa madai hayo.

Suala hili ni zito kubwa sana kwa Taifa, na kama kweli haya yaliyotokea tume ilipaswa kutoa hadharani tasisi zote za usalama zilizoshindwa kutimiza wajibu wao hadi kupelekea kukawa na vikundi hivi.

### v. Kuendelea Kutumia hoja za Kisiasa zisizo na majibu halisi

Aidha, Tume imeeleza kuwa baadhi ya waandamanaji walilipwa fedha na kudai kuwa ilipokea ushahidi wa kiapo kutoka kwa mmoja wa waandamanaji. Kwa

mantiki ya kawaida, ushahidi wa kiapo unapaswa kubainisha wazi mhusika aliyetoa fedha hizo. Hata hivyo, katika hali isiyoeleweka, Tume haijaweka wazi ni nani aliyetoa fedha hizo, wala malengo ya ufadhili huo, licha ya kudai kuwa na ushahidi huo wa kiapo.

Kwa ujumla, hoja hizi ni muendelezo wa hoja za kisiasa zilizotolewa wakati wa uchanguzi na  zinaonyesha kuwepo kwa mapungufu makubwa katika kutoa majibu ya kina kuhusu madai mazito yaliyowasilishwa, jambo linaloibua maswali juu ya ukamilifu na uwazi wa ripoti yenyewe. Tume imekiri zipo sababu za msingi za vijana kuandamana na haiwezekani tena fedha au ufadhili kutoka nje ndio uwe sehemu iliyochangia maandamano. Hoja zilizotajwa kuwa chanzo cha maandamano zinajitosheleza kuamsha vijana wenyewe bila kuwa na ushawishi mwingine.

Vilevile, kulikuwa na matarajio makubwa kutoka kwa umma kuhusu madai kwamba kulikuwa na waandamanaji waliokodiwa kutoka nchi jirani kushiriki katika maandamano hayo. Maswali muhimu yalihusu waliingiaje nchini, ni nani aliyewafadhili, na kwa malengo gani. Hata hivyo, licha ya uzito wa tuhuma hizi katika mjadala wa kitaifa, Tume haikutoa maelezo yoyote wala kuchukua msimamo juu ya madai hayo, hali inayozidi kuongeza sintofahamu na kuacha maswali ya msingi bila majibu.

### vi. Kuhusu Idadi za Vifo na Majeruhi

Pamoja na kwamba Tume imetoa takwimu za vifo na matukio mengine kama tulivyoanisha hapo juu , bado takwimu hizi hazijatoa sura kamili ya kilichotokea wakati wa maandamano mwaka 2025. Ushahidi mwingi na mazingiria ulionyesha kulikuwa na matukio mengi ya mauaji wa raia hadi kwenye makazi na hivyo idadi ya watu 518 haiwezi kuwa inadi kamili ya waliouawa.  Kwakuwa Tume imekiri huenda wengine hawakwenda kutoa taarifa za vifo na majeruhi, basi takwimu hizi haziwezi kuwa ndio za mwisho au za kutegemewa sana kwa kuwa bado uchunguzi zaidi wa idadi ya vifo na majeruhi unahitajika.

Pa takwimu hizi zimeshindwa kubainisha ni watu wangapi waliuwa wakiwa kwenye maandamano na ni wangapi waliouwa wakiwa katika makazi yao kwa kuwa watu wengi walijeruhiwa na kuuawa wakiwa majumbani n katika biashara zao.

### vii. Utata wa Miili ambayo haijulikani ilipo

Jambo lingine la kushangaza katika taarifa ya Tume ni kukiri kwamba kulikuwa na miili takribani 39 iliyotambuliwa na ndugu katika vituo mbalimbali vya afya, lakini baadaye ndugu hao walishindwa kuipata, na hadi leo hawajafanikiwa

kuichukua. Hili ni suala zito linalogusa haki za msingi za kibinadamu na utu hasa kwa familia husika.

Kinachotia wasiwasi zaidi ni kwamba Tume haijaeleza ni nani aliyewazuia ndugu kuchukua miili hiyo, hasa ikizingatiwa kuwa vituo vya afya vilivyohusika ni vya umma. Hali hii inaibua maswali muhimu: ni kwa mamlaka gani miili hiyo ilizuiwa, kwa malengo gani, na ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya waliohusika? Badala ya kutoa majibu ya kina, Tume inaonekana kuishia kueleza tatizo hili kana kwamba ni mlalamikaji, bila kuchukua msimamo wa wazi unaoendana na wajibu wake wa kubaini ukweli na kupendekeza hatua stahiki.

Taarifa hii hajaweza kuweka bayana kuhusu swala la watu ambao miili yao haijulikana ilipo. Hii inaonyesha kuwa muundo wa Tume ulichangia watu wengi kuogopa kwenda kutoa taarifa na. hivyo kufanya tume kutoa taarifa huku wengi wakishindwa kwenda kupeleka taarifa zao.

### viii. Tume kushindwa Kufafanua Kuhusu Uhalali na Madhara ya Tamko la IGP

Eneo jingine muhimu ambalo umma wa Watanzania ulitarajia kusikia msimamo wa Tume ni kuhusu uhalali wa tangazo la IGP Wambura lililowataka wakazi wa Dar es Salaam kutoka nje ya makazi yao, na ambalo baadaye lilionekana kutumika katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kutokana na uzito wa suala hili katika muktadha wa sheria na Katiba, umma ulitarajia Tume kutoa ufafanuzi wa wazi kuhusu uhalali wake na athari zake. Hata hivyo, katika hali isiyoeleweka, Tume haikugusia kabisa jambo hili, jambo linaloacha pengo kubwa katika hoja za kisheria na kiutawala.

### ix. Tume kutokuwataja wahusika wa mauaji ya Oktoba 29, 2025

Jambo la mwisho tunalotaka kuliangazia ni kuhusu hatua ya Tume kuepuka kuwataja wahusika wa mauaji ya Oktoba 29, 2025 na kutopendekeza hatua mahsusi za kuwawajibisha. Badala yake, Tume imependekeza kuundwa kwa chombo kingine cha kijinai kitakachopewa jukumu la kushughulikia masuala hayo, ikiwemo kuwabaini na kuwachukulia hatua watuhumiwa wa mauaji hayo.

Hali hii inaibua swali la msingi kuhusu upeo na madhumuni ya Tume yenyewe. Ikiwa Tume ya Mheshimiwa Jaji Chande haikuwa na mamlaka ya kushughulikia masuala ya kijinai, je, ilikuwa inachunguza nini hasa? Na ikiwa ilikuwa inapokea ushahidi wa mashahidi, hata kwa njia ya viapo, ushahidi huo ulikusudiwa kutumika kwa lengo gani? Kukosekana kwa majibu ya wazi katika masuala haya kunazua shaka juu ya ufanisi na mwelekeo wa kazi ya Tume,

pamoja na uwezo wake wa kufikia matarajio ya umma katika kubaini ukweli na kuhakikisha uwajibikaji.

Muda mwingi umepita na fedha nyingi zimetumika, kwanini Tume imeshindwa kuja na majibu kamili ili kuweza kumaliza swala hili kwa wakati. Kuanza tena mchakato wa uchunguzi ni kupoteza muda, kutokujali yaliyotokea na kuongeza tena mafuta kwenye moto unaowaka. Na ndio maana toka mwanzo tulidhani ni vyema kuwa na tume huru na shiriki ambayo itatumia muda mchache kuja na majibu kamili na ushauri kwa taifa kuhusu yaliyotokea 2025. Tusipokuwa makini tunaweza kwenda hadi uchaguzi ujao tukiwa na swala hili na changamoto zote kuendelea kubakia.

## 3.0 Msimamo na Wito wetu

Kwa kuzingatia maelezo ya uchambuzi huu wa AZAKI, ni wazi kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto za kimuundo zinazohitaji majibu ya kina na ya muda mrefu. Hata hivyo, changamoto hizi pia zinatoa fursa muhimu ya kufanya mageuzi ya msingi katika mifumo ya uongozi, uchumi na mshikamano wa kijamii. Huu si wakati wa kutafakari tu, bali ni mwito wa kuchukua hatua madhubuti za mageuzi. Mustakabali wa Tanzania unategemea uwezo wa kukabiliana na changamoto hizi kwa ujasiri, kujenga mifumo yenye haki, na kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata fursa ya kushiriki katika maendeleo ya Taifa.

Hivyo, AZAKI tunatoa msimamo na ushauri ufuatao kwa maslahi ya haki, uwazi na mustakabali wa taifa:

a) Hatuungi mkono pendekezo la kuundwa kwa chombo kingine cha kijinai kushughulikia masuala yaliyobainishwa na Tume. Tunaamini kuwa Tume ya Mheshimiwa Jaji Chande ilikuwa na uwezo na mamlaka ya kushughulikia masuala hayo, na kwamba kukwepa kufanya hivyo kunaashiria ukosefu wa utashi wa kisiasa badala ya ukosefu wa uwezo. Muda umekwenda na gharama kubwa zimetumika, kwa sasa ipatikane tume huru ya Kutafuta Ukweli, Uwajibikaji na Maardhiano ya Kitaifa. Tume hii iundwe na watu huru na Tume ya Jaji Chande itoe taarifa kamili yenye ukweli halisi hadharani.

b) Tunatambua kuwa kiini (anatomy) cha vurugu na mauaji ya Oktoba 29, 2025 ni mgogoro wa kisiasa ambao umekuwepo Tanzania tangu nchi iliporejea kufuata mfumo wa utawala-kidemokrasia na siasa za ushindani wa vyama vingi 1992 kinyume na shauri wa kitaalam/mapendekezo ya Tume ya Jaji Mkuu Francis Nyalali. Njia ya

kumaliza mkwamo huu siyo kutafuta wachawi – vijana fukara au raia wasiojitambua – bali kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Jaji Nyalali.

c) Serikali ilipe fidia stahiki kwa wahanga wote wa tukio Oktoba, 29, 2025, waliofariki na hata waliojeruhiwa, kwa kuzingatia sheria na mikataba ya kimataifa ya kufidia wahanga. Pendekezo la Tume kuwa 'Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha majeruhi waliopata ulemavu kutokana na ghasia za Oktoba 2025 wanapata huduma za matibabu bure, ikiwa ni pamoja na watakaohitaji vifaa saidizi na viungo bandia (prostheses)' ni kejeli kwa wahanga, ndugu na jamaa zao.

d) Wote waliohusika na mauaji na matumizi ya nguvu kupita kiasi, kama ilivyokiriwa katika taarifa ya Tume, wanapaswa kuwajibishwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria bila upendeleo wowote.

e) Mchakato wa maridhiano ya kitaifa unapaswa kuendana na utaratibu wa viwango vya kimataifa na weledi wa kutanzua migogoro ukisimamiwa na watu waadilifu waliopendekezwa wa wadau wenye maslahi kwenye mgogoro, kuwa jumuishi, ukihusisha makundi yote muhimu ya kijamii na kisiasa, na uongozwe na utashi wa kweli wa kisiasa ili kufikia suluhisho la kudumu. Muda umekwenda na gharama kubwa zimetumika, kwa sasa ipatikane tume huru ya Kutafuta Ukweli, Uwajibikaji na haki kabla ya kuanza mchato wa Katiba mpya.

f) Mchakato wa Katiba Mpya uanze baada ya kupata kwanza muafaka wa Kitaifa na kutolea majawabu na uwajibikaji wa yale yote yaliyotokea mwaka 2025. Katiba mpya iwe sehemu kama sehemu ya kushughulikia chanzo kikuu cha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi na kuzuia kujirudia yasijotokee. Hii iwe ni hatua ya mwisho na Muhimu katika kutelekeza Muafaka wa Kitaifa.

g) Wafungwa wote wa kisiasa wanaoendelea kushikiliwa gerezani kuhusiana na matukio ya Oktoba 29, 2025 waachiliwe mara moja na bila masharti yoyote akiwemo Mwenyekti wa CHADEMA , Tundu Lissu.

h) Watu wote wanaodaiwa kutekwa na kupotea, ambao kwa mujibu wa taarifa ya Tume ni zaidi ya watu 700 na bado hawajapatikana, wanapaswa kupatikana au kuachiwa mara moja bila masharti yoyote. Iwapo wapo waliofariki, basi ndugu zao wapatiwe miili ya wapendwa wao kwa wakati ili waweze kuwazika kwa heshima inayostahili.

i) Tume ya Jaji Chande itoe taarifa kamili kwa umma yenye ukweli halisi hadharani hasa kuhusu mauaji ya watu pamoja na askari waliohusika.

j) Viongozi wote waliozembea na kuupuzia maoni ya AZAKI na watu wengine kuhusu kutatua changamoto hizi na kupata muafaka wa kitaifa kabla ya uchaguzi wawajibishwe ikiwemo Tume ya Uchaguzi kwakuwa imechangia sana changamoto hizi kuelekea uchaguzi wa 2025.

## 6.0 HITIMISHO

Uchambuzi, maoni, mtazamo na msimamo wetu unaoakisiwa katika tamko hili hautofautiani, bali unaendana na maoni, mtazamo na msimamo wa raia wengi kwenye jumuiya, majumbani, maofisini na mahali pa kazi mijini na vijijini, wanaopenyeza sauti zao kupitia jamii ya kiraia na mitandao ya kijamii, wakitamka waziwazi kukataa Ripoti ya Tume ya Uchunguzi wa mauaji, kujeruhiwa na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi mkuu Oktoba 29, 2025. Tunaungana na Watanzania walio wengi kuikataa ripoti hii.

**Taarifa hii imetolewa kwa Vyombo vya habari na:**

1. Legal and Human Rights Centre (LHRC)
2. Tanganyika Law Society (TLS)
3. Centre for Strategic Litigation (CSL)
4. Twaweza EA
5. Affirmative action on Gender Equality Network (AGEN)-Tanzania
6. Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC)
7. Tanzania Transparency Forum (TRAFO), Taasisi Mwenyeji, Kiutawala, wa Tanzania Governance Multi-Stakeholders Group (TG-MSG)
8. Jukwaa la Katiba Tanzania
9. Concern for Development Initiatives in Africa (ForDIA), Taasisi Mwenyeji, Kiutawala, wa Vuguvugu la RAIA Ni SiSi, Tanzania.
10. National Consortium of Civic Education in Tanzania (NACOCET)
11. Muungano wa Vyama Vya Wavuvi Tanzania (FUO)
12. Pastoralists Indigenous Non-Governmental Organizations Forum (PINGOs Forum)
13. Centre Against Gender Based Violence (CA-GBV)
14. Tanzania Child Welfare (TCW)

https://everify.humanrights.or.tz/verify?code=V00VzI